# HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 15 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Mei 2023

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA


# PROF. MSHANDETE AKABIDHI KIJITI KWA DIALLO TFRA



*Aliyekuwa mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Prof. Anthony Mshandete (kushoto) akimkabidhi kitabu cha mafanikio mwenyekiti mpya wa Bodi hiyo Dkt. Anthony Diallo wakati wa hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika tarehe 20.04. 2023 jijini Dar es Salaam.*

NDANI>>


BODI MPYA TFRA YAPATIWA MAFUNZO KUANZA UTEKELEZAJI MAJUKUMU 4



Watakaohujumu mpango mbolea za ruzuku kushughulikiwa 6



Watumishi TFRA washerehekea Siku ya Wafanyakazi Duniani 2023 10

# Prof. Mshandete akabidhi kijiti Kwa Diallo TFRA



Aliyekuwa mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Prof. Anthony Mshandete (kushoto) akimkabidhi kitabu cha mafanikio mwenyekiti mpya wa Bodi hiyo Dkt. Anthony Diallo wakati wa hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika tarehe 20.04. 2023 jijini Dar es Salaam.

Aliyekuwa mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA ) Prof. Anthony Mshandete amekabidhi kijiti cha uenyekiti kwa Dkt. Anthony Diallo huku akijinasibu kwa mafanikio lukuki yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2019 hadi 2022.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika mwezi Aprili 2023, katika ofisi za Makao Makuu ya TFRA jijini Dar es Salaam, Prof. Mhandete aliipongeza bodi mpya ya wakurugenzi kwa kuteuliwa na kuwataka kuendeleza mambao yote mazuri yaliyofanywa na bodi iliyopita.

Akimkabidhi mwenyekiti wa bodi mpya kitabu cha mafanikio ya Bodi iliyomaliza muda wake, Prof. Mshandete aliyataja mafanikio yaliyopatikana kuwa ni pamoja na upatikanaji wa Muundo wa Utumishi, Maendeleo ya Utumishi, sambamba na kuongezeka kwa watumish kwa asilimia 88.75.

Prof. Mshandete aliongeza kuwa uanzishwaji wa ofisi za kanda katika mikoa ya Mbeya, Mwanza, Tabora na Arusha umerahisisha utoaji huduma za Mamlaka kwa wadau wake na kuongeza ufanisi.

Alisema ongezeko la watumishi liliwezesha kuanzishwa kwa chama cha wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE), tawi la TFRA, pamoja na Baraza la Wafanyakazi.

Prof. Mshandete alisema Bodi iliyomaliza muda wake



Aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (2019-2022) Prof. Anthony Mshandete akizuzungumza na wajumbe wapya wa Bodi wakati wa hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika tarehe 20.04.2023 jijini Dar es Salaam.

# Prof. Mshandete akabidhi kijiti Kwa Diallo TFRA



Mwenyekiti mpya wa Bodi ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Anthony Diallo akizungumza na wajumbe wa bodi wakati wa hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika tarehe 20.04.2023 jijini Dar es Salaam .

ilifanikiwa kuanza utekelezaji wa ujenzi wa maabara kwa kutumia fedha za ndani kupitia utaratibu wa Force Account.

Aliongeza kuwa kukamilika kwa maabara hiyo kutasaidia kufanya uchambuzi wa mbolea kwa wakati na kwa ubora unaokubalika.

Katika kipindi cha miaka mitatu Mamlaka ilifanikiwa kuongeza viwanda vya mbolea na visaidizi nchini kutoka 12 hadi 16 kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Kituo cha Uwekezaji.

Mwenyekiti mpya wa Bodi ya wakurugenzi ya TFRA Dkt. Diallo alisema bodi yake itahakikisha inafanya kazi kwa ufanisi ili kuiendeleza tasnia ya mbolea iweze kuwa na mchango katika kukuza uchumi wa taifa.

Dkt. Diallo aliishukuru bodi iliyomaliza muda wake kwa mafanikio hayo yaliyopatikana na kuandikwa kwenye kitabu na kwamba hilo ni jambo zuri la kuigwa ambalo hata bodi yake italifanya pindi itakapomaliza muda wake.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo ( wa kwanza kulia) akitoa maelezo mafupi kuhusu utendaji kazi wa bodi iliyopitia (2019 -2022) chini ya mwenyekiti wake Prof. Anthony Mshandete wakati wa hafla fupi ya makabidhiano jijini Dar es Salaam

# BODI MPYA TFRA YAPATIWA MAFUNZO KUANZA UTEKELEZAJI MAJUKUMU



Wajumbe wa Bodi mpya ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) wakiwa katika mafunzo ya kupatiwa uelewa wa majukumu yao yaliyofanyika jijini Dar es Salaam kuanzia tsrehe 17 hadi 18, Aprili 2023.

Bodi mpya ya Wakurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imepatiwa mafunzo yanayolenga kuwaandaa kutekeleza majukimu yao mapya.

Mafunzo hayo yaliyoendeshwa na Chuo cha Uongozi yamefanyika jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 17 - 18, Aprili 2023.

Akiwasilisha mada kuhusu miongozo mbalimbali ya Ofisi ya Msajili wa Hazina inayosimamia Taasisi za Umma mtaalamu wa uchambuzi kazi

Bi.Rebecca Mahenge amesema wajumbe wa Bodi wanatakiwa kuifahamu miongozo hiyo katika kufanya maamuzi yao.

Bi Mahenge amesema kuwa baadhi ya miongozo ya kuwasaidia wajumbe wa bodi kufanya kazi zao kwa ufanisi ni pamoja na mwongozo wa utendaji wa wajumbe wa Bodi, mwongozo wa tathmini ya utendaji kazi wa Bodi na mwongozo unaoelezea mipaka ya kiutendaji kati ya Bodi na Menejimenti.

Akifungua mafunzo hayo awali, Mwenyekiti wa Bodi



# BODI MPYA TFRA YAPATIWA MAFUNZO KUANZA UTEKELEZAJI MAJUKUMU



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA Dkt. Stephan Ngailo akifafanua jambo wakati wa mafunzo ya wajumbe wa Bodi kuhusu wajibu wa Menejimenti katika kutekeleza dhima na Mpango Mkakati wa Taasisi .

ya Wakurugenzi ya TFRA Dkt. Anthony Diallo aliwataka wajumbe wa Bodi kujielimisha na kuzingatia mafunzo hayo ili waweze kuisimamia Taasisi hiyo kwa mujibu wa sheria kanuni na taratibu.

Dkt Diallo amesema kuwa ni muhimu wajumbe wakayafahamu majukumu yao vema ili waweze kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi.

Akiwasilisha mada kuhusu Utawala Bora mwezeshaji kutoka Chuo cha Uongozi Charles Senkondo amesema mapambano dhidi rushwa, matumizi sahihi ya rasilimali za taasisi na kutokutumia vibaya madaraka waliyopewa wajumbe ni nyenzo muhimu za kukuza utawala bora.

Senkondo amesema kuwa baadhi ya wajibu wa Wajumbe wa Bodi ni kusimamia masuala ya kimkakati ya Taasisi ili kufikia dhima iliyowekwa na Mamlaka.

Ameongeza kuwa, majukumu mengine ya Bodi ni pamoja na kufanya maamuzi yao kwa haki na kwa maslahi mapana ya Taasisi na Taifa kwa ujumla.

Senkondo amesisitiza kuwa ni vema wajumbe wa Biodi wakajiepusha na maslahi binafsi na kutokuwa na mgongano wa maslahi wanaposimamia majukumu waliyopewa.



# Watakao hujumu mpango mbolea za ruzuku kushughulikiwa

Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imetoa tahadhari kwa watakaojaribu kuhujumu mpango wa utoaji wa Mbolea ya Ruzuku kwa wakulima kwa njia mbalimbali za udanganyifu ikiwemo kutoa taarifa zisizosahihi.

Kauli hiyo ilitolewa tarehe 12 Aprili, 2023 Jijini Dar es salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dkt. Stephen Ngailo wakati akitoa taarifa ya maandalizi ya msimu wa Kilimo 2023/2024 sambamba na mikakati ya kuimarisha usajili wa wakulima, upatikanaji na usambaji wa Mbolea.

Dkt. Ngailo alisema kuwa malengo yao mpaka kufika msimu wa 2024/2025 kuhakikisha wanasajili wakulima wapatao Mill 7 katika nchi nzima.

Aidha Dkt Ngailo alisema TFRA itaendelea kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Ili kuhamasisha wakulima kwa njia mbalimbali kujisajili Kwenye Mfumo wa Ruzuku kufuatia utekelezaji na utatuzi wa changamoto mbalimbali za utekelezaji wa Mpango huo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania-TFRA Dkt Stephen Ngailo akitoa taarifa ya maandalizi ya msimu wa Kilimo 2023/2024 sambamba na mikakati ya kuimarisha upatikanaji na usambaji wa Mbolea katika mkutano wake leo na waandishi wa Habari jijini Dar es salaam.



Mwenyekiti wa Kamati ya Ruzuku kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania-TFRA Louis Kasera akizungumza na waandishi wa habari akitolea ufafanuzi mikakati ya kuimarisha upatikanaji na usambaji wa Mbolea.(Picha na Mussa Khalid)

"Katika kutekeleza Azma ya serikali, Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa inaendelea kusajili wakulima, kutumia Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC), kuandaa Ramani ya Mtandao wa usambazaji wa mbolea nchini na kuainisha maeneo ambayo hayana wafanyabiashara na kuchukua hatua stahiki"alisema Dkt. Ngailo

Kuhusu uhuwishaji wataarifa za usajili wa wakulima, Dkt. Ngailo amewataka wakulima nchini kuhakikisha kuwa wanajitokeza kwa wingi kujisajili kwa wakati ili kuwawezesha

# Watakao hujumu mpango mbolea za ruzuku kushughulikiwa

kunufaika na mbolea ya ruzuku inayotolewa na Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema katika msimu wa 2023/2024 usajili wa wakulima unalenga kusafisha au kuhuisha taarifa za mkulima na kufikia maeneo ambayo hayakufikiwa msimu wa mwaka 2022/2023

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Ruzuku, Louis Kasera alisema kuwa, mipango yao ni kuhakikisha kila mkulima anapata kadi yake ili aweze kutambulika kwa urahisi na mashamba aliyonayo.

Pia amewasihi wakulima kutoa taarifa sahihi na kuepukana na udanganyifu kwani atakayebainika atachukuliwa hatua kali.

Hata hivyo serikali imesema itahakikisha kuwa, ifikapo Julai mosi mwaka huu mbolea zote zipatikane katika maeneo yote nchini ili kuwawezesha wakulima kununua mbolea kabla ya msimu kuanza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania-TFRA Dkt Stephen Ngailo akitoa taarifa ya maandalizi ya msimu wa Kilimo 2023/2024 sambamba na mikakati ya kuimarisha upatikanaji na usambaji wa Mbolea katika mkutano wake leo na waandishi wa Habari jijini Dar es salaam.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ruzuku kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania-TFRA Louis Kasera akizungumza na waandishi wa habari akitolea ufafanuzi mikakati ya kuimarisha upatikanaji na usambaji wa Mbolea.(Picha na Mussa Khalid)

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania-TFRA Dkt Stephen Ngailo (kushoto) pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Ruzuku kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania-TFRA Louis Kasera (kulia) wakizungumza na jijini Dar es salaam.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania-TFRA Dkt Stephen Ngailo (kushoto) pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Ruzuku kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania-TFRA Louis Kasera (kulia) wakizungumza na jijini Dar es salaam.



Mkurugenzi wa mauzo na masoko wa kampuni ya mbolea ya Exporting Trade company (ETG) Bw. Manoj Singh akizungumza na Wajumbe wa bodi ya wakurugenzi wa Mamlaka ya udhibiti wa mbolea Tanzania (TFRA), walipo mtembelea ofisini kwake Posta jijini Dares salaam siku ya jumatano Tarehe 19/04/ 2023 ikiwa ni sehemu ya ziara ya wajumbe wapya wa bodi kujifunza na kujitambulisha kwa wadau wa TFRA



Kiongozi wa msafara wa wajumbe wa Bodi ya wakurugenzi Mamlaka ya udhibiti wa mbolea Tanzania (TFRA) Patrick Mwaonenge (kulia) akisisitiza jambo na Mkurugenzi wa kampuni ya mbolea ya OCP Tanzania Bw. Hillary Pato (kushoto) wakati bodi ya wakurugenzi wa mamlaka ya udhibiti wa mbolea Tanzania (TFRA) walipo mtembelea ofisini kwake Osterbay jijini Dares salaam siku ya jumatano Tarehe 19/04/ 2023 ikiwa ni sehemu ya ziara ya wajumbe wapya wa bodi kujifunza na kujitambulisha kwa wadau wa TFRA



Wajumbe wa bodi ya wakurugenzi wa Mamlaka ya udhibiti wa mbolea Tanzania (TFRA), wakizungumza na mkurugenzi wa Dar es salaam corridor group (DCG) alipo kuwa akiwaonyesha namna DCG wanavyo fanya kazi kwenye kupokea na kuhifadhi mbolea siku ya jumatano Tarehe 19/04/ 2023 ikiwa ni sehemu ya ziara ya wajumbe wapya wa bodi kujifunza na kujitambulisha kwa wadau wa TFRA



Wajumbe wa bodi ya wakurugenzi wa Mamlaka ya udhibiti wa mbolea Tanzania (TFRA), Wakipata maelezo kuhusu hatua iliyo fikiwa kaitika ujenzi wa maabara ya uchambuzi wa mbolea kutoka kwa Mwenyekiti wa ujenzi wa maabara hiyo Bw. Joseph Charos(wa kwanza kushoto) siku ya jumatano Tarehe 19/04/ 2023 ikiwa ni sehemu ya ziara ya wajumbe wapya wa bodi kujifunza na kujitambulisha kwa wadau wa TFRA

# Watumishi TFRA washerehekea Siku ya Wafanyakazi Duniani 2023

"Watumishi TFRA washeherekea Siku ya Wafanyakazi Duniani 2023 na kushiriki maandamano ya siku hiyo muhimu yaliyofanyika kwenye viwanja vya Uhuru Jijini Dar es Salaam ambapo kauli mbiu ya mwaka huu ilikuwa "Mishahara Bora na Ajira za Staha ni Nguzo kwa Maendeleo ya Wafanyakazi" Wakati ni Sasa.







# Watumishi TFRA washerehekea Siku ya Wafanyakazi Duniani 2023







# Watumishi TFRA washeherekea Siku ya Wafanyakazi Duniani 2023








# Watumishi TFRA washeherekea Siku ya Wafanyakazi Duniani 2023








Wafanyabiashara 21 wa Mbolea Mkoani Arusha wamejengewa uwezo juu ya elimu ya matumizi sahihi ya mbolea katika mafunzo yaliyofanyika ukumbi wa mikutano wa CEDHA Uliopo Jijini Arusha tarehe 24 na 25 Aprili, 2023 na kutunukiwa vyeti vya ushiriki kwenye mafunzo hayo.



